# TANZANIA BASKETBALL FEDERATION : MPANGO MKUU WA UTEKELEZAJI 2022-2025

| NA. | KIPAUMBELE | JITAHADA | | MAELEZO | VIASHIRIA VYA UFANISI | | SHABAHA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| P1 | **Kuimarisha uongozi na uwezo wa taasisi.** | P1.1 | Kuimarisha na kusimamia Utawala bora na uwajibikaji | Kuimarisha utendaji wa shirikisho kwa kusimamiautawala bora na uwajibikaji kwa watendaji pamoja na viongozi katika ngazi zote kuanzia kwenye vilabu, mikoa mpaka taifa. | P1.1.1 | Idadi ya vyama vya mikoa vilivyokamilisha chaguzi na muundo uliokamilika | | |
| | | | | | P1.1.2 | Idadi ya vilabu vilivyokamilisha chaguzi na muundo uliokamilika | | |
| | | P1.2 | Kuimarisha na kusimamia nidhamu ya kazi na maadili ya uongozi | Ili kuhakikisha malengo ya shirikisho yanafikiwa kuna umuhimu wa kuimarisha na kusimamia nidhamu na maadili ya viongozi katika ngazi zote za mchezo kuanzia vilabuni, mikoani mpaka taifa hii itajenga sura ya mchezo pamoja na kuvutia wadau kushiriki katika maendeleo ya mchezo. | P1.2.1 | Idadi ya mashauri ya kinidhamu yaliyofanyiwa kazi | | |
| | | P1.3 | Kuhakikisha uwepo wa wa ofisi na watumishi wa shirikisho. | Kulingana na mahitaji yanayo endelea kuongezeka kutokana na kukua kwa mchezo ni muhimu kuhakikisha Shirikisho linakuwa na ofisi zake rasmi pamoja na watumishi ambao watasaidia kuziendesha shughuli za kila siku kwa wakati bila ucheleweshaji wowote. | P1.3.1 | Ofisi za shirikisho | 1 (DSM) | SG |
| | | | | | P1.3.2 | Wafanyakazi wa kuajiriwa | Wawili (2) | SG |
| | | P1.4 | Kujenga uwezo kwa mikoa na vilabu | Ili kuhakikisha kiwango cha mchezo kinakuwa bora Shirikisho kwa kushirikiana na wadau mbali mbali litawajibika kukuza na kuendeleza kiwango cha ufundishaji, uamuzi na usimamizi wa mchezo katika ngazi zote za mchezo.<br><br>Vilabu kuwa na viongozi imara waliojengewa uwezo ndio vitachagiza kupata viongozi bora wa mikoa ambao nao watasaidia kupata viongozi bora wa kitaifa.Ili kikapu kiwe na uhakika na mafanikio ya kweli na ya muda mrefu ni muhimu kuwepo kwa programu endelevu za kuwajengea uwezo viongozi wachanga ili kupata mwendelezo wa uhakika wa kiutawala. | P1.4.1 | Idadi ya Katiba zilizo rasimishwa kwenye mikoa/vilabu. | | |
| | | | | | P1.4.2 | Idadi ya mikoa/vilabu vilivyo kamilisha usajili. | | |
| | | | | | P1.4.3 | Idadi ya akaunti za benki kwa mikoa/vilabu zilizo funguliwa. | | |
| | | | | | P1.4.4 | Idadi ya kozi za kiutawala kwenye mchezo kwa mikoa/vilabu. | | |
| | | P1.5 | Kuhakikisha uwepo wa kanuni na taratibu zitakazo saidia ufanisi katika utendaji wa shirikisho | Kama majukumu ya katibu mkuu yanavyotambulika kikatiba kuwa ni mtendaji mkuu wa shirikisho hivyo itakuwa ni wajibu wake kuhakikisha malengo na madhumuni ya viongozi wa shirikisho yanatekelezeka kwa vitendo Kwa kutumia kanuni na taratibu zitasaidia kufikika kwa malengo iliyojiwekea kwa ufanisi.Hili litaendana na mbinu za kisasa za kiutawala katika kusimamia na kuendesha majukumu ya kitaasisi. | P1.5.1 | Idadi ya kanuni na taratibu za kuendesha na kusimamia shughuli za shirikisho kitaifa. | 5 | SG |

| NA. | KIPAUMBELE | JITAHADA | | MAELEZO | VIASHIRIA VYA UFANISI | | SHABAHA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | P2.1 | Ujenzi wa miundombinu ya mpira wa kikapu (Ofisi na viwanja) | Kuhakikisha shirikisho linakuwa na sehemu maalum ya kufanyia shughuli zake kwa kushirikiana na wadau kujenga ofisi za shirikisho pia ili kuhakikisha kuwa mchezo unasambaa zaidi kwenye jamii shirikisho litajenga viwanja vyenye hadhi mbali mbali ili kukidhi mahitaji mbali mbali ya wadau wake. | P2.1.1 | Idadi ya viwanja vilivyojengwa | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **P2** | **Kuboresha miundombinu ya mpira wa kikapu na mazingira ya kuchezea.** | **P2.2** | Kufungua kanzidata ya wachezaji,makocha,waamuzi na viongozi. | Kufungua kanzidata (database) ya wachezaji , makocha, waamuzi na viongozi ambayo itatunza taarifa zao za kimchezo ambazo zitasaidia na kutumika kwa ajili ya shughuli za kimanendeleo ya mchezo pamoja na kuweka mikakati ya kuendeleza wachezaji.<br><br>Taarifa hizi zitatoa fursa kwa wawekezaji kujua kiwango cha uhitaji wafursa mbalimbali za kielimu na kiajira zilizopo au zitakazo hitajika kwa siku za baadae.pia taarifa hizi zitasaidia kujua sifa halisi za wachezaji kama umri, urefu, historia, elimu na historia yao. | **P2.2.1** | Idadi ya mikoa iliyo kamilisha kweka taarifa za wachezaji, makocha, waamuzi na viongozi kwenye TBF Map | | ALL COMMISSONERS |
| | | **P2.3** | Kuweka utaratibu wa BIMA ya afya kwa wachezaji wa Timu za taifa. | Kuanzisha utaratibu wa kuwa na Bima ya Afya kwa wachezaji wote wa Timu ya Taifa kwa kuunda ushirikiano na mashirika ya BIMA na kupata unafuu na baadae kulsambaza kuwafikia wachezaji wa mikoa hadi kwenye vilabu. | **P2.3.1** | Idadi ya timu zilizo katiwa BIMA ya wachezaji (Timu za Taifa) | | |
| | | | | | **P2.3.2** | Kiwango cha gharama za BIMA kitakacho lipiwa | | |
| | | **P2.4** | kusimamia viwango na ubora katika  mchezo. | Kusimamia viwango na ubora katika mchezo ili kuupa nafasi ya kuutangaza na  kuuza mchezo kwa wadau mbali mbali ndani na nje ya nchi. | **P2.4.1** | Idadi ya kanuni za kuongoza michezo ya 5x5,3X3 na Wheelchair basketball | | |
| | | | | | **P2.4.2** | Idadi ya makongamano/semina au mafunzo ya kujenga uwezo wadau kuelimishwa kuzielewa kanuni. | | |
| | | **P2.5** | Kujenga utamaduni wa kikapu. | Kujenga utamaduni wa kikapu kwa kizazi kijacho ambacho kitanufaika na programu mbali mbali za kuendeleza mchezo kwa kuzingatia madili bora kwa vijana kimchezo, kijamii na kielimu. | **P2.5.1** | Idadi ya jitihada mbali mbali za kijamii (i.e. CSR, Makongamano ya Kitaaluma, Ubunifu , Mavazi , etc) | | MIPANGO |
| | | **P2.6** | Kuanzisha programu mbali mbali za kubadilishana uzoefu. | Kuanzisha programu za kubadilishana wachezaji na makocha kati ya shirikisho na washirika mbalimbali kama sehemu ya kubadilishana uzoefu pamoja na kujifunza namna mbali mbali za kuongoza mchezo. | **P2.6.1** | Idadi ya programu zilizofanyika | | |
| | | | | | **P2.6.2** | Idadi ya wanufaika walio patikana | | |

| NA. | KIPAUMBELE | JITAHADA | | MAELEZO | VIASHIRIA VYA UFANISI | | SHABAHA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **P3** | **Kuboresha utoshelevu wa kifedha na mazingira ya uwekezaji.** | **P3.1** | Kubuni njia mbali mbali za kuongeza vyanzo vya mapato kwa shirikisho. | Ili kuweza kulisaidia shirikisho kujiendesha na kumudu gharama zake mbali mbali za kiutendaji ni muhimu kulisaidia shirikisho kwa kushirikiana na wadau mbali mbali kubuni na kuwezesha upatikanaji wa njia mbadala za kujipatia mapato kupitia mchezo.<br><br>Kama ada, tozo, udhamini, ruzuku ya serikali, gawio,faida na mapato ya huduma mbali mbali zitakazoweza kutolewa na shirikisho kwa kushirikiana na wadau. | **P3.1.1** | Idadi ya mikataba ya udhamini/ufadhili | | |
| | | | | | **P3.1.2** | Idadi ya programu mbali mbali za maendeleo ya mchezo za kulipia | | |
| | | | | | **P3.1.3** | Kiwango cha ruzuku toka serikalini kendeleza mchezo. | | |
| | | | | | **P3.1.4** | Mapato yatokanayo na huduma mbali mbali zinazotolewa kupitia mchezo (i.e. betting loyalty fees , etc.) | | |
| | | | | | **P3.1.5** | Mauzo ya biadhaa zitokanazo na nembo, rasilimali zingine zitokanazo na mchezo. (i.e. apparels, items, etc.) | | |
| | | | | | **P3.1.6** | Mapato yatokanayo na matangazo kwa njia ya kimtandao kupitia mitandao ya kijamii. | | |
| | | | | | **P3.1.7** | Mapato yatokanayo na ada za ushiriki mashindano mbali mbali ya kitaifa | | |
| | | | | | **P3.1.8** | Mapato yatokanayo na leseni za wachezaji , makocha, waamuzi na wadau wengine wa mchezo. | | |
| | | | | | **P3.1.9** | Mapato yatokanayo na ada za kuendesha mashindano mbali mbali ya kitaifa/kimataifa | | |
| | | | Kusimamia na kuratibu uandaaji wa mpango wa bajeti na matumizi bora ya fedha za shirikisho. | Mojawapo ya njia bora za matumizi ya fedha za shirikisho ni kuhakikisha, kusimamia na kuratibu matumizi yote kulingana na mipango na bajeti iliyo andaliwa kwa kushirikisha vyombo vya shirikisho kama kamati ya utendaji, bodi na mkutano mkuu. | **P3.2.1** | Kuandaa,kupitisha na kutumia kanuni za mapato na matumizi ya shirikisho. | Kanuni za mapato na matumizi ya shirikisho | TG |
| | | | | | **P3.2.2** | Idadi ya mikoa iliyopokea mafunzo ya njia bora za kuandaa mahesabu na kutoa ripoti zake. | | TG |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | P3.2 | | | P3.2.3 | Idadi ya wahasibu wanaosimamia vyama vya mikoa kutunza hesabu zao | | TG |
| | | | | | P3.2.4 | Ripoti ya ukaguzi ya Fedha za Shirikisho | Audited Financial Reports | SG & TG |
| | | | | | P3.2.5 | Idadi ya ripoti za fedha kwa kila robo ya mwaka | Quatrely Financial Reports | SG & TG |

| NA. | KIPAUMBELE | JITAHADA | | MAELEZO | VIASHIRIA VYA UFANISI | | SHABAHA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| P4 | **Kukuza nembo na taswira ya mpira wa kikapu kitaifa na kimataifa.** | P4.1 | Kupanua wigo wa ushirikiano na wadau katika kukuza mchezo kupitia programu mbali mbali. | Kukua kwa mchezo kumeongeza wigo wa ushirikiano na wadau ambao kupitia programu zao watalisaidia shirikisho kupunguza gharama za uendeshaji wa majukumu yake kupitia utekelezaji wa programu husika.<br><br>Programu mbali mbali kama za kuendeleza vipaji kwa watoto na vijana, watu wenye ulemavu , maendeleo ya wanawake, elimu ya awali kwa walimu wa MCHEZO ili kuhakikisha nchi inakuwa na vipaji vingi katika nyanja zote za mchezo. | P4.1.1 | Idadi ya mikataba ya ushirikiano kimkakati (i.e. vyuo, makampuni, mawakala , vituo vya michezo , taasisi za kijamii , taasisi za kiserikali , taasisi za kimataifa ,etc) | | |
| | | P4.2 | Kuboresha mahusiano kati ya shirikisho na wadau (i.e. serikali , vyama vya kitaalamu, taasisi na makampuni). | kuhakikisha malengo ya shirikisho yanafikiwa au kufanikishwa kwa kukuza na kuboresha mahusiano na wadau yatafanikisha utekelezaji wa majukumu ya shirikisho katika ngazi zote za nchi (i.e. Kitaifa, Kimkoa hadi katika ngazi ya vilabu).<br><br>Serikali kama mdau mkuu wa Shirikisho litahakikisha mawasiliano na taarifa zote za msingi kwenda na kurudi yanatekelezeka kwa wakati na kwa ushirikiano/uadilifu. | P4.2.1 | Idadi ya vyama vya kitaalamu vinavyo sajiliwa na kujiunga na shirikisho. | | |
| | | | | | P4.2.2 | Idadi ya maelekezo/ mapendekezo toka Serikalini yaliyofanyiwa kazi (i.e.BMT/Wizara) | | |
| | | | | | P4.2.3 | Idadi ya taasisi / kampuni zinazoshirikiana na shirikisho | | |
| | | P4.3 | Kuimarisha na kuendeleza mahusiano ya Shirikisho kimkoa, kitaifa, kikanda na kidunia | Kwa kutambua umuhimu wa mahusiano kwenye ngazi mbali mbali za shirikisho katika kuimarisha fursa za mchezo kupitia masomo (scholarships), ajira, ushiriki (PARTICIPATION), MAFUNZO (CLINICS) na nyinginezo ambazo zitawanufaisha wadau wa mchezo kama wachezaji, walimu, waamuzi na viongozi. | P4.3.1 | Idadi ya mikutano /kozi /kliniki / makongamano kati ya shirikisho na vyama vya kimataifa i.e. FIBA, FIBA ZONE V kikanda iliyofanyika kwa wadau wake (i.e. | | |
| | | | | | P4.3.2 | Idadi ya mikoa yenye uongozi unaotambulika rasmi kwenye serikali za mikoa yao. | | |
| | | P4.4 | Kukuza na kuendeleza mahusiano kati ya Shirikisho na Serikali pamoja na taasisi zake | Serikali ni mdau wa kwanza katika maendeleo ya michezo hapa nchini kupitia sera na sheria mbali mbali zinazolenga kukuza na kusimamia maendeleo ya michezo hasa kikapu. hivyo ni wajibu wa shirikisho kukuza na kuendeleza mahusiano bora na serikali kwa manufaa ya mchezo. | P4.4.1 | Idadi ya maelekezo/ mapendekezo toka Serikalini yaliyofanyiwa kazi (BMT/Wizara) | | |
| | | | | | P4.4.2 | Idadi ya sera na miongozo toka Serikalini (i.e. taasisi zake) inayolenga kuboresha mazingira ya mchezo. | | |
| | | | | | P4.4.3 | Idadi ya programmu za pamoja zinazotekelezwa kati ya Serikali na Shirikisho kupitia taasisi zake. | | |
| | | P4.5 | Kutumia utalii wa kimichezo kama njia ya mapato na kutangaza nchi na mchezo. | Kuangalia njia bora ambayo shirikisho litaweza kutumia utalii wa michezo kuwa ni chanzo cha kipato kama shirikisho pamoja na kuitangaza nchi na mchezo. | P4.5.1 | Idadi ya watalii waliopatikana kupitia mchezo | | |
| | | P4.6 | Kuanzisha kitengo cha habari na mahusiano | Kuanzisha kitengo maalumu kitakacho simamia utoaji na upatikanaji wa taarifa rasmi za shirikisho kwa wadau pamoja na mahusiano.<br><br>Taarifa hizi zitatolewa katika aina mbalimbali kama picha, video au nyaraka kupitia njia mbali mbali. | P4.6.1 | Upatikanaji wa Afisa habari na Mahusiano wa Shirikisho | | |

| NA. | KIPAUMBELE | JITAHADA | | MAELEZO | VIASHIRIA VYA UFANISI | | SHABAHA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | P5.1 | Kusimamia na kuendeleza program mbalimbali za timu za taifa | Kuhakikisha Tanzania inarudi kwenye ramani ya kimataifa kuna umuhimu wa Kusimamia na kuendeleza programu mbalimbali za Timu ya Taifa (Wakubwa na watoto), wanaume na wanawake na kwa watu wenye ulemavu kupitia mikakati mbali mbali itakayowekwa. | P5.1.1 | Uwepo wa Mkurugenzi wa Ufundi atakayesimamia programu ya timu ya taifa. | Mkurugenzi wa Ufundi | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **P5** | **Kuongeza programu na mipango ya maendeleo kwa vijana, wanawake, na watu wenye ulemavu.** | | timu za taifa | | **P5.1.2** | Uwepo wa mpango wa maendeleo ya timu ya taifa | Mpango wa Maendeleo | |
| | | **P5.2** | Kuanzisha mafunzo kwa walimu katika mashule (i.e. msingi na sekondari). | Kufundisha mafunzo ya awali kwa walimu wa shule za msingi na sekondari nchi nzima TBF kuimarisha kamisheni ya walimu wa kikapu kwa kushirikiana na serikali kuhamasisha viwanja vya mchezo wa mpira kikapu vinajengwa kwenye shule za misingi na sekondari. | **P5.2.1** | Idadi ya walimu wa shule za msingi na sekondari walio pokea mafunzo ya awali. | | |
| | | | | | **P5.2.2** | Idadi ya viwanja vilivyo jengwa katika shule za msingi na sekondari | | |
| | | | | | **P5.2.3** | Makubaliano ya kutoa mafunzo ya mchezo kwa walimu/wanafunzi kupitia chuo cha michezo Malya. | Mkataba wa Makubaliano | |
| | | | | | **P5.2.4** | Idadi ya makocha/wakufunzi watakaoweza kutoa mafunzo ya mchezo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari nchini. | | |
| | | **P5.3** | Kuanzisha programu za maendeleo ya wachezaji. | Kuanzisha na kusimamia programu mbali mbali zitakazolenga kumsaidia mchezaji mmoja mmoja kisaikolojia, elimu ya afya , ujasiriliamali na elimu ya fedha. | **P5.3.1** | Idadi ya programu zilizo anzishwa | | |
| | | | | | **P5.3.2** | Idadi ya wachezaji walio nufaika | | |
| | | | | | **P5.3.3** | Mgawanyo wa kijinsia na wa watu wenye mahitaji maalumu ya wachezaji walio nufaika | | |